

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA HAMSINI NA NNE

20 JUNI, 2018



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA HAMSINI NA NNE – TAREHE 20 JUNI, 2018

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**457. MHESHIMIWA STANSLAUS SHING'OMA
MABULA (NYAMAGANA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana linalojengwa katika Kata ya Mkolani limechukua zaidi ya miaka minne sasa bila kukamilika:-

- (a) Je, Serikali haioni kuwa na miradi isiyokamilika kwa wakati kunarudisha nyuma maendeleo;
- (b) Je, ni lini sasa Serikali itapeleka fedha za kukamilisha jengo hilo.

**458. MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kituo cha Afya Mlandizi kimetimiza vigezo vyote vya kuwa Hospitali ya Wilaya:-

Je, ni lini sasa Serikali itapandisha hadhi Kituo hicho kuwa Hospitali ya Wilaya.

**459. MHESHIMIWA EDWIN MGANTE SANNDA
● (KONDOA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wananchi wa Vijiji vya Hurumbi, Dumi na Chandimo (Kata ya Serya), Ausia, Mulua na Guluma (Suruke) pamoja na Hachwi, Kutumo na Chora (Kolo) katika Jimbo la Kondoa Mjini, Kijiografia wana changamoto kubwa ya huduma muhimu za afya ambapo wanalazimika kufuata huduma hizo katika Zahanati za jirani au Hospitali ya Mjini:-

Je, ni lini Serikali itatupatia *Mobile Clinic* kutatua changamoto hii.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

460. MHESHIMIWA AZZA HILLAL HAMAD (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Bwawa la umwagiliaji katika Kijiji cha Ishololo katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

461. MHESHIMIWA MUSSA BAKARI MBAROUK (TANGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, kwa nini Serikali isianzishe utaratibu wa kupima mizigo na usajili wa abiria katika vyombo vyote vya majini kama inavyofanyika 'Air Port' ili kuepusha ajali za mara kwa mara.

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

462. MHESHIMIWA ANNA JORAM GIDARYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Kituo cha Wazee Sarame kilichopo Magugu Wilaya ya Babati Vijijini ni Kituo cha muda mrefu ambacho kinahudumiwa na kusimamiwa na Wizara ya Afya. Kituo hiki kina changamoto nyingi ikiwemo uhaba wa Watumishi, usafiri wa dharura, huduma ya kwanza, Vifaa Tiba na miundombinu ya barabara:-

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma zote za msingi katika Kituo hicho hasa ikizingatiwa kuwa Wazee wengi ni walemavu wa Viungo, Vipofu, Waliopooza na Viziwi pia.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

463. MHESHIMIWA DKT. RASHID MOHAMMED CHUACHUA (MASASI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Jeshi la Polisi katika Wilaya ya

Masasi halina nyumba za makazi wala usafiri kwa muda mrefu sana:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea Askari hao nyumba za kuishi kwa sababu nyumba wanazoishi sasa zimechakaa sana na pia hazitoshelezi mahitaji yao;

(b) Je, ni lini Serikali itawapatia usafiri wa uhakika Askari hao ili waweze kusimamia usalama wa raia na mali zao kwa uhakika.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

464. MHESHIMIWA DEVOTHA MATHEW MINJA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Serikali iliahidi kutaifisha mashamba makubwa ya uwekezaji yasiyoendelezwa:-

Je, mpaka sasa mashamba mangapi yametaifishwa.

III. HOJ21A ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
20 JUNI, 2018**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**